**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI SERIKALINI (GPSA)**

**HOTUBA YA**

**MHE. WAZIRI WA FEDHA**

**DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA**

**KATIKA UZINDUZI WA MFUMO WA GIMIS NA MAJENGO MAPYA YA WAKALA**

**JIJINI DODOMA**

**TAREHE 21/10/2023**

**Mh. George Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;**
**Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha;**
**Waheshimiwa Mawaziri wenzangu mliopo hapa;**

**Dkt. Natu El-maarmy Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, na Mlipaji Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Jenifa Omolo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha;**

**Bi. Amina Shaaban, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha;**

**Bw. Elijah Mwandumbya, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha;**

**Makatibu Wakuu mliopo hapa;**

**Bi. Dorothy Stanley Mwanyika, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini;**

**Prof. Geraldine Arbogast Rasheli, Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini;**

**Viongozi na menejimenti ya Wizara ya Fedha;**

**Watendaji wa Taasisi zinazosimamia ununuzi wa Umma;**

**Wageni waalikwa;**

**Mabibi na mabwana;**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania …….**

Awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa wenye afya njema.

Kipekee kabisa, naaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na maelekezo yake ambayo ndio msingi wa utendaji kazi wetu wakati wote, Mhe. Rais amekuwa na dhamira ya dhati kabisa katika kuwaletea maendeleo wananchi kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa kuendelea kuchochea shughuli za uzalishaji na uwekezaji katika maeneo mbalimbali. Tunamshukuru sana na tunampongeza sana.

Ninatambua Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ni moja ya Taasisi zinazosimamia sekta ya ununuzi nchini, na ni Taasisi ya kimkakati iliyoanzishwa ili kukidhi mahitaji ya Serikali katika sekta ya ununuzi wa umma. Wakala tangu ulipobadilishwa kutoka Bohari kuu ya Serikali mwaka 2008 umekuwa ikiendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi licha ya changamoto mbalimbali.

Lengo la kuanzishwa kwa Wakala ni kuisaidia Serikali kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali Kuu, Taasisi, Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali na kujiendesha kwa faida. Serikali inaona mafanikio makubwa ambayo yanachangiwa na Wakala katika Uendeshaji wa

shughuli za kila siku za Serikali. Kuna maeneo mengi ambayo Wakala umefanikiwa na maeneo ambayo yana changamoto pia bado yapo.

**Mwenyekiti wa Bodi**, nitoe pongezi kwa kutekeleza agizo la Serikali kwa kutoa taarifa kwa Mamlaka za Serikali na kuhabarisha umma wa watanzania utekelezaji wa shughuli za Wakala ili wapate taarifa kuhusu utekelezaji wa masuala mbalimbali ndani ya Serikali. Hatua hii ni nzuri na naomba iendelee ili kuhahakisha umma wa watanzania unapata taarifa kwa wakati. Serikali yetu imechukua hatua mbalimbali katika kuboresha sekta ya ununuzi wa umma kwa maslahi mapana ya Taifa ikiwa ni pamoja na marekebisho ya Sheria ya ununuzi wa umma ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za ununuzi kwa urahisi kulingana na wakati uliopo.

**Mwenyekiti,** nimesikia katika taarifa yako ya utekelezaji wa mpango mkakati kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2018/19 – 2022/2023 kuwa pamoja na mambo mengine mmefanikiwa kuongeza mapato kutoka bilioni 13.9 mwaka 2018/2019 hadi kiasi cha bilioni 31.7 mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la 127%, na mmefanikiwa kujenga mfumo wa kieletroniki ujulikanao kama GIMIS na pia, mmefanikiwa kujenga majengo mapya katika mikoa sita (6) ikiwa ni hatua ya kuboresha ustawi wa wafanyakazi katika eneo la kazi.

**Mwenyekiti**, pamoja na kukamilika majengo ya ofisi na vituo vipya vya mafuta vya Songwe, Simiyu, Pwani na Dodoma pia, mmeeleza kuhusu kufanya ukarabati katika ofisi za mikoa 17 na kusimika matenki ya mafuta

katika mikoa 12, hatua hizi sio tu zinaongeza mapato lakini pia zinaongeza morali ya utendaji kazi na kuonesha utendaji kazi wenu.

**Mwenyekiti,** ninawapongeza sana kwani Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inasisitiza sana matumizi ya mifumo ili kurahisi utendaji kazi na kuongeza ufanisi. Taarifa hii inaonyesha kuwa Wakala ni Taasisi inayotekeleza mipango yake kama ilivyojiwekea. Ninawapokeza sana Bodi kwa usimamizi na nawapongeza sana menejimenti na watumishi kwa utekelezaji huu.

Hizi ni hatua kubwa katika usimamizi wa rasilimali na uendeshaji wa Taasisi za umma kwa kuwa msingi mkubwa wa mafanikio ni kutekeleza yale ulijipangia kwa ufanisi.

**Mwenyekiti**, nimefarijika na taarifa yako kuwa licha ya utekelezaji wa mambo mengi katika kipindi cha miaka mitano lakini Wakala uliendelea kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali na mpaka kufikia mwaka 2022/2023 mmechangia kiasi cha Tshs. bilioni 11.9. Hongereni sana

Ni imani yangu mtaendelea kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ili Serikali iweze kutekeleza mipango mbalimbali iliyojiwekea.

Naomba niwapongeza na kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika ujenzi wa mfumo nikianza na Mamlaka ya Serikali Mtandao akiwa ndio

mjenzi wa mfumo huu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge , Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi. Naomba pia, niwashukuru wadau walioshiriki katika ujenzi wa majengo mapya nikianza na Shirika la Nyumba la Taifa akiwa ndio mbunifu na mjenzi na SUMAJKT akiwa ndio mshauri mwelekezi.

**Mwenyekiti**, umeeleza utendaji kazi wa mfumo na umetaja faida za mfumo huu kwa Wakala na Taasisi nunuzi. Kimsingi majukumu yote ya Wakala yanatekelezwa ndani ya mfumo huu, na hivyo bila shaka umerahisisha na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yenu. Pia, umeeleza kuwa mpaka sasa mfumo huu umeunganishwa na mfumo wa GePG na unatarajiwa kuunganishwa na mfumo wa MUSE, GAMIS, NeST na Single window. Kwa kuwa Mhe. Rais – Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza mifumo ya Serikali kusomana ninaelekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kuhakikisha wanaunganisha mfumo wa NeST na GIMIS haraka iwezekanavyo kwa kuwa mfumo huu unatumiwa na Wizara, Mashirika ya Umma, Wakala, Ofisi za mikoa na Halmashauri za Wilaya nchini katika kupata huduma za GPSA. Ninaelekeza pia mifumo mingine ihakikishe inaunganishwa na GIMIS ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Wakala.

Wito wangu kwa Taasisi nunuzi kuhakikisha wanatumia huduma za GPSA kwa kuwa sheria ya ununuzi na kanuni zake inatutaka kupata huduma na vifaa mtambuka kupita GPSA.

**Mwenyekiti**, ni imani yangu kuwa katika mpango mkakati wa Wakala kwa mwaka 2022/2023 hadi 2027/2028 mtatekeleza kwa kiwango kikubwa zaidi na kupiga hatua kubwa katika utoaji wa huduma kwa Serikali na Taasisi zake. Aidha, mmeonesha kujipanga vyema kukabiliana na mabadiliko ya hali ya nchi na hivyo inatupa faraja kuwa Wakala huu utakuwa endelevu na unaokabiliana na mabadiliko ya teknolojia.

**Mwenyekiti**, nawashukuru kwa kunialika katika uzinduzi wa mfumo wa kieletroniki (GIMIS) na majengo mapya yaliyojengwa katika mikoa ya Dodoma, Pwani, Simiyu na Songwe.

Naomba nitamke rasmi kuwa mfumo wa GIMIS na majengo manne ya ofisi nimeyazindua rasmi leo tarehe 21 Oktoba, 2023.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**